# *WAKATI WA KUUNGANA NA ISHARA YAKE*

Habari za jioni. Majaliwa kuwa hapa usiku wa leo, na kusimama mahali hapa.

2 Mimi, asubuhi ya leo, nikishuka kuja barabarani... Nilikuwa nimetoka kwenda kuomba, nikimngojea Bwana. Na nilipokuwa nikishuka kuja barabarani, nilifungua re—redio ya mhudumu mmoja, Ndugu Smith, yule ndugu mweusi, (je! nyote mlimsikia asubuhi ya leo? Yeyote wenu?) huko, ninaamini ni Ohio. Mtu fulani alikuwa akiniambia kuhusu yeye akihubiri, na akasema, "Unapaswa kufungua umsikilize, namna hiyo."

3 Ilitukia tu nilimpata, asubuhi ya leo. Na bila shaka alikuwa akisema juu ya vile dhambi ilikithiri kwa wingi duniani leo, naye alikuwa... Ndipo nikaendelea mbele kidogo, kituo cha pili, na nikashuka nikamsikia mwingine. Wakati nilipofika hapa, nilikuwa karibu tayari kuona kama haikuwa nimechelewa sana kuja kanisani, asubuhi ya leo nilipoingia. Kwa hiyo, kweli tumependelewa sana kuwa hapa usiku wa leo, na kutumika katika ibada ya Bwana.

4 Na tukizungumza juu ya Ndugu Neville, na ule ujumbe hivi majuzi, kwa maskini mama huyu mdogo, dada yetu ambaye ndio kwanza aondoke kwetu. Huyo alikuwa, sote tunajua yeye alikuwa ni nani, ni Dada Weaver. Na nikifikiria juu ya mtu mmoja hapa, atakayebatizwa usiku wa leo; dada... Nilimbatiza dada huyo kwenye kidimbwi hiki wakati mimi... iliwabidi wamlete hapa katika kiti cha magurudumu. Alikuwa anakufa, kwa kansa, naye alikuwa na usiku huo tu wa kuishi; madaktari walikwisha kumkatia tamaa, alikuwa atakufa kesho yake asubuhi. Nami nilienda nyumbani mwake na kujaribu kuzungumza naye kuhusu uponyaji wa Kiungu, naye akaendelea tu kurudia, "Sistahili uje chini ya paa langu." Akasema, "Si—sistahili kwa mhudumu kuwa katika nyumba yangu." Akasema, "Mimi ni mwenye dhambi." Lakini akasema, "Bwana, sitaki kufa namna hii." Na kwa hiyo Grace Weber, hapa juu, alinipeleka kule. Nilikuwa ndiyo kwanza niingie, nimechoka kutokana na mikutano; na hapo nilipokuwa nikimwombea, na kumsomea Maandiko, naye akaokoka. Ndipo, ilikuwa ni vigumu kwake kuinua mkono wake juu, bali alitaka kupeana mikono na kila mtu. Alininii tu... jambo fulani lilimpata.

5 Na walipokuwa wakipeana mikono, niliona ono lake akienda kwenye kizimba cha kuku, akirudi. Nikasema, "Vema, itakuwa sawa sasa"; na hiyo ni miaka kumi na nane iliyopita. Naye

amekuwa hatua moja kubwa mbele ya hiyo kansa, wakati huo wote. Kama alikufa, . . . Hakufa akiwa na kansa yoyote, alikuwa na ugonjwa wa moyo na ukamwua. Walikuwa wamemweka chini ya oksijeni; alikufa kwa ugonjwa wa moyo.

6 Na halafu nilikuwa nikiwazia, wakati tu wa mwisho hapo watu walipokuwa wakitoka, nao wakaimba, *Ndipo Yesu Akaja*. Hivyo ndivyo ilivyotukia hasa, Yeye alikuja na kuyaokoa maisha yake kwa miaka hiyo kumi na nane. Nami nikawazia, jinsi unavyofaa. Mwanamke huyo labda hakujua alikuwa akifanya hivyo. Halafu, tena, huenda alijua. Lakini jinsi ilivyofaa kuwa na sehemu hiyo pale, *Ndipo Yesu Akaja*.

7 Sasa kidogo ni mapema, na—natumaini, mwanzo wangu mkuu kwa ajili ya mikutano. Ninashikwa na wasiwasi sana. Asubuhi ya leo, nilikuwa nimechanganyikiwa sana, nilikwenda ku—kuomba. Na ni—niko nyumbani, nimerudi hapa. Familia, ndiyo kwanza niwapeleke Arizona, nami ninaninii . . . kusudi watoto waende shuleni. Na mimi nimerudi hapa ku—kupumzika tu kwa namna fulani, niende nikawinde pamoja na Ndugu Wood na kundi la ndugu hapa; niende nikawinde, juma hili lijalo. Tunashuka kwenda huko Kentucky. Nami nilikuwa . . . nimekuwa katika . . . ilitokea tu kwamba nilikuja katika siku ambayo—ambayo Bibi Weaver alikufa, na ni vema tu kwamba ningeweza kuwa hapa na kumsaidia Ndugu Neville katika mazishi hayo.

8 Nami sijaribu kuninii . . . Sijaribu ku—kusema mengi sana kuhusu jambo hilo, mwajua, karibu na watu wanaonung'unika. Kwa sababu, nafikiri, moja ya mambo ya kuchukiza sana ni kuona mwa—mwanamume ama mwanamke ambaye daima ananung'unika. Daima nimewazia, "Mungu, nikinge na jambo hilo." Unaona, hilo—hilo huidhoofisha imani wakati wote, mwajua. Unaninii tu—unaninii tu . . . kama ukininii—kama ukininii . . . Ninajua wanapokuwa wazee, kila mmoja wetu, tutafanya jambo fulani kutukia na jambo fulani litatukia. Na ninajua vitu hivyo vidogo vitaendelea kuongezeka, hiyo ni kadiri unavyozidi kuwa mzee, havina budi kuongezeka tu. Lakini nafikiri moja ya mambo ya kuchukiza sana, ni kwa Shetani kuyatia taji maisha ya mtu fulani: maskini mwanamume ama mwanamke mzee mkorofi, unaona. Na—natumaini ya kwamba sitafikia mahali hapo. Natumaini ya kwamba ninaweza kustahimili jambo hilo, mizigo yangu, na—na kufikia mahali ambapo . . . Ninataka maisha yangu yatiwe taji kwa Utukufu wa Mungu: Uvumilivu Wake, upole, amani, unyenyekevu, na kujazwa na Roho Mtakatifu.

9 Nami . . . moja ya mambo yangu muhimu ambayo daima yameniudhi kote maishani mwangu, limekuwa ni hali ya wasiwasi. Kwamba wakati ninapokuwa mchovu sana, ndipo ninakuwa dhaifu sana. Ninakuwa . . . kwa namna fulani unajisikia kana kwamba hakuna mtu anayekujali, unajua, na—

na unakuwa ninii kabisa . . . Unao, pia. Na mimi inatokea tu kwamba nina kipimo kilichozidi kiasi chake, wajua, na inakuwa mbaya sana wakati mwingine, na ni vigumu kwangu . . . Ni hangaiko, na hilo ndilo linalousababisha. Nami ninafikia ambapo basi mara nyingi, hasa sana kukiweko na hayo maono mengi sana, unaona, unanipata tu. Ninamwangalia mtu, ninawazia, "Hili ni ono. La, la, la, si ono. Naam! Silo?" Unaona? Nawe kamwe hutambui hiyo inaambatana na gharama ya jinsi gani. Kwa hiyo basi—kwa hiyo basi u—unashangaa. Ndipo unaanza kufikiri, "Vema, wewe unaninii . . . " Ndipo unajirudia na kusema, "Vema, sasa, ni—nimefanya nini? Mimi hapa, ni—nina umri wa miaka hamsini na sijamfanyia Bwana kitu; na ni—ninazeeka. Na ni nini . . . ? Loo, jamani." Ndipo unapata tu ninii . . . kile tulichozoea kuita "kuudhika." Baadhi yenu ndugu wa karibu rika yangu mnakumbuka kile walichozoea kuita "kuudhika." Baba alizoea kuzungumza kuhusu jambo hilo nami nikashangaa alimaanisha nini, na hakika sasa ninajua alichomaanisha. Kwa hiyo basi, unaanza kujisikia hivyo, ambapo si hata moja ni kweli; ni wewe tu, unajua hivyo. Unaona, unajua hivyo, ni wewe tu unayefanya jambo hilo.

10 Kwa hiyo nilikuwa nikijaribu kujituliza mwenyewe kidogo sasa, na kuwa tayari kwa ajili ya—ya msukumo mkubwa ambao ninatumaini unakuja karibuni. Na halafu kupitia . . . Inanipasa kwenda New York mara moja, nami . . . kwenye mkutano huko, kampeni. Kisha nishuke niende Shreveport, halafu nirudi huko Phoenix. Halafu nije upande wa magharibi . . . kwenye mpaka wa kusini wa Marekani. Halafu wanafanya matayarisho kwa ajili ya nchi za ng'ambo sasa, itakayoanza mara tuwezapo baada ya mwanzoni mwa mwaka, labda Machi, Aprili, kitu kama hicho; ambapo unaanzia huko Stockholm ama Oslo, kisha uzunguke ulimwenguni, kama tunaweza kwenye ziara hii inayofuata.

11 Na sasa niko nyumbani, kwa namna fulani nikipumzika kidogo, nipate kujirudia kwa namna fulani na kupata afya. Na kama Bwana akipenda, nitarudi Jumapili ijayo, kutoka huko Kentucky. Na—na endapo ni sawa, inampendeza Bwana, na Ndugu Neville hajali; vema, nitajaribu tu kuchukua ibada Jumapili ijayo, kama Bwana a—akipenda. Na kama Yeye yuko radhi kabisa kama Ndugu Neville anavyoridhia, ni—nitakuwa hapa. Naam bwana, Yeye yuko tu . . . kama Yeye yuko radhi kabisa kuhusu hilo kama Ndugu Neville anavyoridhia. Natumaini anaridhia. Sasa, unaona, basi najua hivi karibuni, Bwana akipenda, nitawaacha nisafiri kwa muda mrefu.

12 Na mimi . . . jumbe ndogo tu, ninapochukua kitu kidogo moyoni mwangu, ndipo na—na—najisikia kama ninataka kuwaelezea hicho, unaona, na tunaweza kushirikiana kwenye hicho. Sasa, nina chache ya hizo, tano ama sita ambazo ndiyo kwanza zinijie katika siku chache zilizopita. Na nilikwenda, siku chache hapa, kuwinda kindi sehemu hizi huku. Na ninaingia

mwituni, na ninachukua penseli na karatasi. Unaona? Sasa yapata wakati kunapopambazuka vizuri, ninaegemea mtini mahali fulani. Kama silali, ninaanza kuomba, na ndipo mimi, Bwana atanipa jambo fulani, ninaanza kuandika mihtasari midogo yake, unaona. Mnajua ninalomaanisha; unapokuwa peke yako, na halafu unaninii. . . Ndipo mimi hapa ninaingia, ninayaandika yote kwenye padi ya karatasi. Na ndipo wakati ninapoitwa, ninakimbia na kuchukua padi yangu na kuanza kuupitia na kuona ninachoweza kuanzia, unaona. Hilo ndilo lililotukia sasa hivi.

13 Kwa hiyo sasa, ninataka kuninii, Bwana akipenda, kuzungumza tu. . . Ninajaribu kufanya. . . kukatiza hizo jumbe kubwa, ndefu, unaona; ambapo zinakuchukua saa nyingi. Na Bwana alinisaidia kufanya kazi nzuri fupi ya hizo huko Chicago, usiku wa mwisho kule, kama dakika thelathini. Ndipo mtu fulani alinikaribia, akasema, "Sikudhani ilikuwa ndani yako, bali ulifaulu!" Kwa hiyo dakika thelathini, kutoka kwenye kama saa mbili na nusu, ama tatu, wajua. Kwa hiyo labda ninaweza kuharakisha usiku wa leo na kupata mazoezi kidogo, nisiwashikilie kwa muda mrefu sana.

14 Mungu awabariki. Haidhuru niende wapi, kamwe hakutakuwa na mahali kama maskani hii hapa. Ni nyumbani, nyumbani panapopendeza. Nami nasikitika pamoja na familia ya Weaver, na pia pamoja na ndugu huyu mweusi wa thamani aliyekufa, niliomba pamoja naye muda mfupi kabla hajaaga dunia, na ni mtu mzuri. Naye yuko Nyumbani pamoja na Mungu sasa, na yote yamekwisha. Na mtu huna budi kuaga dunia hata hivyo, nasi sote tunajua jambo hilo. Kwa hiyo sisi tunaninii. . . Bwana na aweke nafsi zao katika amani, na siku moja tunatarajia kujiunga pamoja nao katika Nchi moja huko ng'ambo, ambako hakuna magonjwa, huzuni, wala mauti. Hadi wakati huo, hebu na tufanye yote tuwezayo kwa ajili ya Injili.

15 Nikizungumza juu ya wasiwasi, nilikuwa nikiomba juu ya jambo hilo asubuhi ya leo. Ungefanyaje kama usingekuwa na wasiwasi? Wazia tu jambo hilo. Wasiwasi ni sehemu ya maisha. Hilo kwa namna fulani lilinitia moyo wakati nilipowazia hilo. Kama usingalikuwa na wasiwasi, ungekuwa kama mwanasesere wa tambaa, usingekuwa na hisia zozote. Hakuna kitu ungaliweza kukifanyia kazi. Kama vile mume na mke, pengine kama mke anataka kufanya jambo fulani, nao wanajaribu kufanya kazi pamoja (hususan Wakristo), na huyo mwingine anataka. . . Na halafu mnapokuja pamoja kuninii. . . na ukaona yale aliyofanya; anakuta. . . Unaona, wasiwasi kweli unawaleta karibu zaidi. Na mtu fulani anakwambia ya kwamba "Vema," kasema, "wazia tu juu ya maskini yule mke aliyeshikwa na wasiwasi sana wakati wewe hukuwa mzuri sana, ama mume alivyopitia kwenye wasiwasi wakati wewe hukuwa mzuri sana. Ndipo wakati yote yamesamehewa, angalia jinsi ulivyojisikia

kumhusu yeye. Jamani, ulininiii tu . . . ” Unaona, huna budi kuwa na wasiwasi. Hivyo tu.

16 Na hebu wazia tu, juu ya hisia, vipi kama hukuwa na hisia yoyote, huna maumivu wala chochote kile? Vipi kama kusingalikuwako na maumivu hata kidogo? Usingekuwa na hisia hata kidogo. Unaona? Na kama hukuwa na hisia yoyote, basi moja ya hisia zako ingekuwa imekwisha. Unaona? Kwa hiyo, unaona, kila kitu ni sawa tu hata hivyo. Kwa hiyo, “Mungu, tupe tu neema kulistahimili jambo hilo,” jambo ndilo hilo. Kama tukisimama tu na neema hiyo, na kusimama pale na kusema, “Tunajua ya kwamba maisha haya yatakapokwisha, yaliyo makuu zaidi yako kwenye ng’ambo ya pili ambako tunatarajia kwenda.” Na sasa, tu—tunakumbuka ya kwamba mambo haya yote, huo ni wasiwasi.

17 Watu wengine wanajaribu kuutambulisha Ukristo, ya kwamba “wewe uko huru na wasiwasi. Uko. . . ” La, huko huru. “Uko huru na hangaiko.” Loo, la! Unaongeza hangaiko unapokuwa Mkristo, kwa sababu kwa namna fulani ovyo—ulitangatanga, hukujali, vyovyote ilivyokuwa huko nje, bila kujali ulichofanya.

18 Lakini wakati umekuwa Mkristo halisi, kila wakati unajiuliza, “Je! ninamfurahisha Bwana wangu? Laiti ningaliweza kusikia kutoka Kwake!” Inakutia wasiwasi, inakufanya ujihadhari. Hicho ndicho kinachokufanya ulivyo wewe. Kwa hiyo basi, wasiwasi ni baraka. Ni vile tu unavyoliangalia jambo hilo. Ni vile tu unavyoliangalia jambo hilo. Unaona? Kama ukiangalia tu upande ule mwingine, kuna ninii—kuna ninii. . .Haidhuru unakikata kitu kipande chembamba jinsi gani, ungali una pande mbili zake, unaona. Kwa hiyo unataka kuona pande zote mbili.

19 Kwa hiyo wasiwasi. . .Nafikiri, “Loo jamani, ni. . .Huu wasiwasi ni kitu gani? Kama ningalizaliwa bila wasiwasi huu.” Vema, kama nisingalikuwa na wasiwasi huu, nisingalikuwa jinsi nilivyo. Nisingalikuwa Mkristo, labda. Wasiwasi huu ndio ulionisukuma kwa Yesu Kristo. Unaona? Kwa hiyo, umekuwa ni kitu chenye baraka kwangu mimi.

20 Kwa hiyo basi kama Paulo alivyosema, kama kwamba wakati alipokuwa na wasiwasi ama jambo fulani au chochote kile, alikuwa amemsihi Bwana ku—kumwondolea mara tatu. Ndipo Bwana akasema, “Sauli. . .Paulo Wangu, neema Yangu yakutosha.”

21 Yeye akasema, “Basi, nitapendezwa na udhaifu wangu. Basi niwapo dhaifu, nina nguvu.” Unaona? Mradi tu ni kwa mapenzi ya Mungu, sawa.

22 Sasa, nilimsihi Yeye wakati mmoja wakati ulikuwa ukinisumbua sana, uliniogopesha. Naye akaniambia, yapata miaka minane ama kumi iliyopita, alisema, “Hautakutisha

tena." Na haujapata kunitisha kamwe. La, bwana; sina—sina wasiwasi juu ya jambo hilo. Ninausikia tu, bali ninajua uko hapo; bali ninaendelea tu kwa sababu haunitishi tena, ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Sasa, Yeye angaliweza kusema, "Hautakuwako tena," sawa tu na kusema "Hutatishika tena."

23 Kwa hiyo ni mapenzi Yake kwamba jambo hilo linatukia, kwa hiyo ninalikumbatia tu na kusema, "Asante, Bwana, nitatembea hivyo."

24 Sasa, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa—kwa maombi. Je! kuna haja maalum ya maombi? (Naona leso zimewekwa hapa.) Inua mkono wako. Bwana, bariki kila mmoja wa watoto Wako.

25 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokaribia Kiti Chako kikuu, kitukufu cha neema, kwa kuwa tumeombwa kuja. Tunakuja kwa kuitwa na Yesu Kristo. Na tunakuja na fadhaa zetu zote, na kumtwika Yeye kwa maana Yeye anajishughulisha sana nasi. Hiyo ni faraja kuu ya jinsi gani, kujua ya kwamba Yeye anajishughulisha sana nasi. Mungu mkuu wa Mbinguni, Muumba; anajishughulisha sana nasi, viumbe Vyake. Tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hilo, Bwana. Ni faraja ya jinsi gani katika nyakati hizi tunazoishi, wakati inaonekana haiwezekani ku—kupata faraja kutoka kwa kitu chochote ila Neno Lako. Hiyo ndiyo faraja yetu, ni Ahadi Yako. Na katika Ahadi Yako, ulisema maombi yetu yajulikane, na "Mkiomba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Na Ahadi hizi zote kuu: "Ombeni nanyi mtapewa. Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka, basi utang'oka." Ahadi hizi zote, nasi tunaweza kuchota kutoka kwenye Hilo yoyote tu tanayoomba.

26 Mikono iliinuliwa, wanahitaji jambo fulani, Bwana. Wewe unajua haja zao; wape, Baba. Ninaweka maombi yangu pamoja na yao mbele Zako, mkono wangu ukiwa umeinuliwa pamoja na yao. Hapa kwenye dawati hili hapa, kuna leso zilizowekwa hapa. Loo, jinsi ambavyo watu wenye imani, imani thabiti, Bwana, . . . Inaonekana kuwa ni kitu fulani tu ambacho umenibariki nacho, kuweza kuwaombea wagonjwa. Popote, mahali popote, kokote niendako, ni jambo fulani kuhusu kuwaombea wagonjwa. Mungu, saidia sasa. Ninaomba kwa uaminifu ya kwamba Wewe utajibu maombi ya leso hizi ambazo zimewekwa hapa, kwa ajili ya watu walioomba. Jalia rehema Yako iwe juu yao.

27 Bwana, tunasikia ya kwamba Dada Hicks ana mwanamke fulani hapa, ambaye aliruka kuja hapa kwa ndege kutoka mahali fulani apate kuombewa, akiwa na kansa; naye alitaka kujua kama angeweza kumleta hapa. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utayahifadhi maisha ya mtu huyo; tujalie. Mpwa wangu mdogo, Mikie, amelala huko hajiwezi na anatapika, akiwa na homa kali; ndiyo kwanza aondoke mlangoni. Bwana, na—naamini tulikuwa

na maombi ya imani pale ambapo uliikomesha, na ni—ni—ninakushukuru Wewe, nikiihisi hiyo homa ikimwacha mvulana huyo kabla sijaondoka mle chumbani.

28 Sasa, Bwana,. . .na tunakushukuru kwa ajili ya mambo haya yote. Sasa kura imeniangukia kuzungumza juu ya Neno Lako. Tupe Neno Lako, Bwana. "Neno Lako ni Kweli." Bariki nafsi zetu na utupe ne—neema tunayohitaji, tupate kuchota kutoka kwenye Ahadi za Mungu usiku wa leo, katika Neno, kutuendeleza sehemu iliyosalia katika juma hili; tujalie. Mbariki mchungaji wetu, mtu huyu hodari, mke wake, watoto wake, mashemasi, wadhamini, na kila mtu anayeingia ama kutoka katika jengo hili; tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba baraka hizi. Amina.

29 Sasa, ninataka kusoma kutoka sehemu mbili za maandiko ya Bwana. Ninataka kusoma kwanza kutoka katika Kitabu cha Zaburi, Zaburi ya 86. Halafu nataka kusoma kutoka katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 16, 1 hadi 3. Na ninataka kusoma sehemu ya Zaburi hii, si yote bali kuendelea hadi kufikia kwenye kifungu cha 11, ambapo kidogo ni zaidi ya nusu yake.

30 Nami ninataka kutangaza jambo hili, kama nikiliita somo, kabla ya kulihubiri: *Wakati Wa Kuungana Na Ishara Yake*. "Ishara ya wakati wa kuungana," hilo linasikika kama ni gumu kufahamika. *Kuungana*; unaona? *Wakati*; wakati wa kuungana, huo ndio ulioko sasa. Na *Ishara* ya huo wakati wa Kuungana.

31 Katika—katika Zaburi, maombi ya Daudi, Zaburi ya 86.

> *Ee Bwana, utege sikio lako unijibu, maana mimi ni maskini na mhitaji.*
>
> *Unihifadhi nafsi yangu, maana mimi ni mcha Mungu.*
>
> *Wewe uliye Mungu wangu, umwokoe mtumishi wako* akutumainiye.
>
> *Wewe, Bwana, unifadhili, maana nakulilia wewe mchana kutwa.*
>
> *Uifurahishe nafsi ya mtumishi wako, maana nafsi yangu nakuinulia wewe, Bwana.*
>
> *Kwa maana wewe, Bwana, U mwema, umekuwa tayari kusamehe, Na mwingi wa fadhili, kwa watu wote wakuitao.*
>
> *Ee Bwana, uyasikie maombi yangu;. . .uisikilize sauti ya dua zangu.*
>
> *Siku ya mateso yangu nitakuita, kwa maana utaniitikia.*

Loo, si hilo linapendeza? "Utaniitikia."

> *Katikati ya miungu hakuna kama Wewe, Bwana, Wala matendo* mfano *wa* tendo lako.

*Mataifa yote uliowafanya watakuja; watakusujudia Wewe, Bwana, watalitukuza jina lako; kwa kuwa ndiwe uliye mkuu,*

*Wewe ndiwe mfanya miujiza, Ndiwe Mungu peke yako.*

Sikilizeni sasa.

*Ee* B*WANA*, *unifundishe njia yako; ni—nitakwenda katika kweli yako; unganisha moyo wangu kulicha jina lako;* (Muungano! Unaona?). . .*unganisha moyo wangu kulicha jina lako.*

32 Ninazungumza sasa juu ya *kuungana;* na *ishara ya wakati.* Sasa, katika mlango wa 16 wa Mathayo Mtakatifu.

*Wakamjia Mafarisayo na Masadukayo,*. . .*kamjaribu,* wakamwomba awaonyeshe *ishara itokayo mbinguni.*

Ndipo *akajibu akawaambia, Kukiwa jioni,* ninyi *mwasema, Ku-*. . .*Kutakuwa na kianga; kwa maana mbingu ni nyekundu.*

*Na asubuhi, mwasema, Leo* kutatanda. . .*dhoruba; kwa maana mbingu ni nyekundu, tena kumetanda. Enyi wanafiki, ninyi mwajua kuutambua uso wa mbingu; lakini, je! Ishara za* zamani *hizi ninyi* hamwezi *kuzitambua?*

Bwana na aongeze baraka Zake za rehema kwenye kusomwa kwa Neno hili.

33 Sasa, tunazungumza juu ya kuungana huku, wakati wa kuungana; ishara ya wakati wa kuungana. Unaona, Yesu alikuwa hapa, katika Maandiko haya ya mwisho tuliyosoma, Yeye alikuwa akiwakemea makasisi kwa kutoweza kuutambua wakati wala ishara ya wakati. Sasa, hilo daima limekuwa ni jambo kubwa kwa watu, unaona, kuweza kutambua i*shara ya wakati unaoishi*; kwa maana Mungu huliandika dhahiri kusudi kusiweko na mtu atakayelikwepa.

34 Sasa, kwa kawaida, ningerudi nyuma na kuchukua kutoka kwa wahudumu wengine, watumishi wengine wa Bwana katika wakati wa Biblia (kama vile ishara ya wakati wa Nuhu, ishara ya wakati wa Danieli na—na kadhalika, ishara mbalimbali), lakini nataka kukwepa hilo usiku wa leo ku—kuokoa wakati, niweze. . .Lakini daima imekuwa ndiyo njia ya Mungu, kuwapa i—ishara ya maumbile ya kawaida ya wakati, kusudi kila mtu ajue tu ilikuwa ni—ni wakati gani. Na Mafarisayo hawa walipaswa kujua wakati wao. Walipaswa kujua ulikuwa ni wakati gani. Yeye alisema mahali pengine, "Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu." Unaona? Ni—ni jambo ku—kubwa sana kwamba tufahamu. Unaona, "Bila ufahamu!"

35 Hiyo ndiyo sikuzote walirejea kwa manabii kuhusu, walisema, "Naye alikuwa na ufahamu, kwa maono kutoka

kwa Bwana. Nalo Neno la Bwana liliwajia ma—manabii wa kale." Unaona, walipata ufahamu kwa Neno la Bwana, kwa manabii. Na halafu basi—manabii walitoa ishara. Kama vile, mtu mmoja alilala kwa ubavu wake kwa muda mrefu sana, kisha akageuka na kulala kwa ubavu huo mwingine. Mtu mmoja ilimbidi kuvua nguo zake. Na loo, kuna mambo mengi waliyofanya kuonyesha ishara waliyokuwa wakiishi kwayo. Na sasa tunajua ya kwamba Mungu aliyeumba mbingu na nchi, na—na kupanga kazi Yake hivi kwamba angeelezea wakati Wake kwa ishara, Mungu yuyo huyo yu hai leo. Kwa hiyo hatuna budi, jambo fulani . . . Tunapoona wa—wakati tunaoishi, hapana budi kuna kitu fulani ambacho mtu fulani anapuuza, mahali fulani. Unaona? Kwa maana Mungu asingeacha mambo haya yatukie bila ya kutupa ishara madhubuti, kwamba ambapo, ambayo—ambayo tungeifahamu.

36 Sasa ndivyo ilivyo siku hizi, kwamba makasisi, hatulisomi vizuri. Ni kama tu vile ilivyokuwa wakati huo, hawakuwazia kwamba wakati ulikuwa umewadia. Wa—waliwaza walikuwa wakiishi kwa amani sana wakati huo, na hivyo basi hawakuwa wakimtazamia Masihi kabisa. Na Yesu amesema ya kwamba kuja Kwake kutakuwa kama "mwizi wakati wa usiku," wakati wa—wakati watu wasingekuwa na habari juu ya Kuja Kwake. Lakini kulikuwa na baadhi ya wanawali waliotoka wakaenda kumlaki, nusu yao, walikuwa na mafuta kwenye taa zao na walikuwa tayari; walikuwa wakingojea ishara hiyo. Na hao ndio ninawazungumzia usiku wa leo, unaona, hao wanaoitafuta ile ishara sasa, ishara ya Kuja Kwake.

37 Ishara hizi zilizotolewa, na Bwana, zinatolewa tu kwa waaminio. Wasioamini kamwe hawaioni. Zinapita moja kwa moja juu yao, wala hawazioni. Na sasa, kwa hakika tu kama ilivyo kwamba Malaika wa Bwana angeweza kusimama juu ya jukwaa hili usiku wa leo, kwa hakika tu kama—kama ninavyowaangalia, na ningeweza kuwa nikimwangalia; ama ungeweza kuwa ukimwangalia wala mimi nisingeweza kumwona, ama ningemwangalia na wewe usingeweza kumwona. Sasa, unajua hayo ni Kimaandiko; hiyo ni Kweli kabisa. Waliona . . . Mnajua Paulo alianguka chini, bali wao . . . hakuna hata mmoja wao angaliweza kuiona hiyo Nuru.

38 Hiyo Nuru ilikuwa pale pale wakati Yohana aliposimama pale mbele ya umati, na maelfu wakiwa kule ukingoni, ya makasisi na—na wenye hekima, watu mashuhuri. Naye Yohana akasema, yeye mwenyewe, alishuhudia akimwona Roho wa Mungu akishuka kama hua na akashuka juu Yake, na Sauti ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Wala hakuna aliyemwona ila Yohana. Unaona? Ilikuwa tu ni kwa ajili yake.

39 Je! uliona jinsi ilivyokuwa dhahiri, ile ishara kwa ajili ya wale mamajusi? Waliangalia, kulikuwa na . . . Walikuwa

Waebrania. Hawakuwa mamajusi hasa wa Kihindi, walikuwa ni Waebrania; kwa maana walikuwa kule katika nchi hiyo wakisoma elimu ya nyota, kumalizia elimu yao. Na wakati walipokuwa . . . walipoangalia kuelekea Yerusalemu, na wakijua ya kwamba waliona hizo nyota tatu kutoka kila moja ya nji—njia zao za kuzaliwa, za Hamu, Shemu, na Yafethi, za koo ambazo wao walitokea, kila mmoja, nao waliona hizo nyota katika njia za kuzaliwa kwao. Hiyo ilikuwa ni ishara kwao, ya kwamba wakati nyota hizo zilipopanga mstari, Masihi alikuwa duniani.

40 Loo, jamani! Si ajabu walikuja, “Yuko wapi? Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tumeiona nyota Yake Mashariki, nasi tumekuja kumwabudu. Yuko wapi?” Walijua ya kwamba huyo mtoto mchanga Masihi alikuwa amelazwa mahali fulani, kwa maana Mungu aliwapa ishara ya wakati, ya kwamba Mungu na mwanadamu walikuwa wakiungana pamoja. Ni muungano wa jinsi gani, wakati Mungu alipojiunganisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu! Mkuu, muungano mkubwa kabisa kuliko miungano yote iliyopata kufanywa, ilikuwa ni wakati Mungu alipoungana na mwanadamu; na kuacha ninii Wake—ukoo Wake mkuu wa kuwa Mungu na akaitandazia hema Yake na kuchukua ubinadamu, na akawa mmoja wao, kuwakomboa. Umoja. Huo nini? Huo ulileta amani kati ya Mungu na mwanadamu milele; jinsi tulivyo na shukrani.

41 Na ishara hazikutumwa . . . Sasa wazia tu, kila mtu, na mamajusi wote; watu wa siku hizo, saa zao zilikuwa ni nyota. Kulikuwa na mlinzi aliyepanda juu ya—ya mnara, naye angepanda kule juu na kushika zamu. Naye aliona wakati nyota fulani zilipokuwa katika makundi fulani, wakati zilipokuwa zikipita, alijua ilikuwa ni saa ngapi. Je! mnakumbuka katika Maandiko, “Ni saa ngapi, mlinzi?” Naye mlinzi akarudi akamwambia ilikuwa ni saa ngapi. Unaona, walishika saa kwa nyota.

42 Sasa, hivi si ni jambo la ajabu ya kwamba nyota hizi zilipanga mstari kabisa kwa ajili ya watu watatu wala hakuna mtu mwingine aliyeona jambo hilo? Unaona? Hakika kabisa kwa utaratibu. Sasa, unaweza kuwa sawa kabisa na Maandiko. Unaona? Wakati hizo nyota zilipoungana, zilipoungana pamoja katika kundi hili, watu watatu pia waliungana pamoja wakati uo huo. Nawe unaweza kuungana sana na Mungu, katika Neno Lake, mpaka mambo haya yanakuwa halisi, nawe unaweza kuyaona na kujua ya kwamba ni ya kweli. Unaona? Ishara ya wakati! Unaweza ukaangalia moja kwa moja upitie juu yake, useme, “Aha, upuuzi!”

43 Bali kwako *wewe* si upuuzi. Kwako, umeungana na Neno, nalo Hili hapa. Ndipo ni—ni Nuru kabisa, Ndugu Pat, wakati—wakati—wakati—wakati unapoona ishara hii ikiungana na mwaminio. Na huyo ndiye ninayemwelekezea hili, ni mwaminio, kwa maana asiyeamini halioni kamwe. Na ingekuwa ni shutuma

jinsi gani kama Yeye angalikuwa yupo duniani leo; kwa wengi wa makasisi wetu leo, ambao hawawezi kuisoma ishara hii; ishara tunazosoma kila siku hapa maskanini, na kuona mambo. Na wengine wanaisoma na kuona maandiko ya mkono kwenye ukuta, na hata hivyo wengi wanaipuuza tu, wala hawaioni hata kidogo. Si kitu kwao hata kidogo; hawaioni.

44 Sasa angalia, kwamba katika jambo hili, ya kwamba Yeye—Yeye alielekeza kwenye ishara za kitaifa. Sasa, wakati walipomwuliza juu ya jambo hili, walitaka ishara; Naye akawapa ishara zilizotukia. Nao walitaka kujua mwisho wa ulimwengu ungekuwa ni lini, ni nini ingekuwa ishara ya wakati wa mwisho. Naye akawaelekeza kwenye sehemu nyingi katika Maandiko kuhusu ishara za taifa, juu ya ishara ya mbinguni huko mbinguni, na ishara ya duniani; Yeye aliwapa ishara nyingi, ishara, ishara nyingi, daima tu ishara fulani. Na wakati alipowaambia pale katika mahali pamoja kuhusu ishara ya taifa, Yeye alisema, "Mtakapoona mataifa, unaona, yakianza kukusanyika kuuzunguka Yerusalemu, unaona, ndipo tunajua ya kwamba wakati wa shida yao umekaribia, mtakapoona Yerusalemu umezungukwa na jeshi."

45 Sasa, kabla kwamba wao hawajafanya jambo hili, Mungu . . . Ulimwengu ilibidi kuungana. Tito, jemadari huyu mkuu wa Kirumi ilimbidi kuyaunganisha majeshi yake pamoja na kusogea karibu, baada ya hawa Wayahudi kuikataa ishara ya wakati huo iliyotolewa na Mungu kwa ajili yao. Hapo ndipo Tito alipoyaunganisha majeshi yake pamoja, na akaja kuuteka mji. Kwanza ilibidi kuwe na muungano wa watu wa Mungu (walivyojiita) dhidi ya Neno la Mungu, kabla taifa hilo halijaweza kujiunganisha lenyewe dhidi ya watu wa Mungu. Unaona, u—u—umoja, muungano; kuungana pamoja.

46 Ninaamini ya kwamba tunaishi katika wakati mkuu wa kuungana. Ninashusha taa hizi nyekundu, na ishara za kimulimuli na kila kitu (cha wanawake, jinsi wanavyofanya; na wanaume, jinsi wanavyofanya; na makanisa, jinsi yanavyofanya), nikilionyesha kundi hili dogo, kwa moyo wangu wote, ya kwamba ninaamini ya kwamba tunapanga mstari kwenye mkondo wa Neno la Mungu katika saa hii kuu ya kinabii, kabla tu ya kuja kwa Bwana Yesu; kuungana pamoja na kuwa tayari.

47 Sasa, unaona, kabla Tito hajayaunganisha mataifa ya . . . majeshi yake pamoja, Israeli waliungana pamoja na kujiunganisha pamoja, ya kwamba wasingemwamini Yesu kwamba ni Masihi. Walimkataa, na kumfukuza, na kumsulubisha. Halafu basi, wakati walipoukataa wokovu waliotumiwa, waliungana pamoja kufanya jambo hilo. Sasa, shikilia hilo mawazoni: kuungana wenyewe pamoja, kuukataa Ujumbe wa wakati huo! Iliwabidi wafanye jambo hilo. Ndipo walipofanya hivyo, ndipo ishara ya taifa ikaingia.

48 Mataifa yalianza kuungana pamoja, naye Tito akaleta jeshi hili kubwa la Warumi na Wayunani na kuzizunguka kuta za Yerusalemu, wakawazingira hao watu mle ndani sasa, nao wakafa kwa njaa. Walikula maganda kutoka kwenye miti. Josephus, yule mwanahistoria mashuhuri, anatwambia. Na wakala nyasi kutoka ardhini. Hata waliwachemsha watoto wao mmoja kwa mwingine na kuwala; unaona, kwa kuwa walikuwa ni wenda wazimu. Na halafu basi wakati, hatimaye, Tito, alikuwa ameketi huko nyuma juu ya milima, kuuzunguka Yerusalemu kule, na—na hao watu mle ndani walidhani walikuwa wakifanya mapenzi ya Mungu, wakati walipoyaona majeshi haya yakiingia. Walikuwa wamekataa kumsikiliza yule Mwalimu Mkuu, Bwana Yesu, akiwaambia jambo hilo.

49 Hakukuwa na mmoja wa hao Wakristo aliyeshikwa mle ndani, kwa kuwa waliona ile ishara nao wakaondoka. Unaona? Walisema, "Walio juu ya dari wasishuke, wala yeye aliye shambani asirudi, asichukue koti lake; bali akimbilie kwenda Yuda, na ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe katika majira ya baridi wala siku ya Sabato." Kwa sababu, kwenye majira ya baridi kali, mi—milima ingejaa barafu; na kwenye siku ya Sabato, mlango, milango ilifungwa, lile lango, nao wangeshikwa katika hali hiyo. Unaona? Tunataka kufikia jambo hilo karibuni sana kuhusu...jinsi ambavyo Mungu hufanya mambo hayo, Bwana akipenda.

50 Angalieni sasa, Yeye...Waliomba ya kwamba ingekuwa hivyo...isiwe hivyo, Yesu aliwaambia waombe kwa ajili ya jambo hilo, wala kamwe hawakumshika mmoja wao mle ndani. Walikuwa wameondoka kwa sababu waliangalia ile ishara, nao wakaondoka; ndivyo mambo yalivyokuwa.

51 Loo, jinsi makanisa siku hizi yanavyopaswa kuona ishara ya wakati tunaoishi! Kimbilieni kwa nguvu mwezavyo mwende Kalvari, kwa ajili ya Uzima; si kwenye kanisa fulani, bali kwa Yesu Kristo. Jiungeni na Yeye, wala si na madhehebu fulani ama kanuni fulani za kanisa. Jiungeni na Kristo, na mwe na hakika ya kwamba ni Yeye. Hamwezi kuchukua tu chochote, hamna budi kuwa na hakika kwamba ni Yeye. Ni wakati wa muungano jinsi gani!

52 Sasa, tunaona ya kwamba walimkataa Masihi halafu wakaungana pamoja na kujiundia shirikisho, na kutoa ho—ho...hoja miongoni mwao ya kwamba mtu yeyote atakayempokea Yesu kama Nabii, ya kwamba watafukuzwa kanisani. Mnamkumbuka yule kijana kipofu aliyekuwa na macho mapofu? Nao wanafunzi wakasema, "Ni nani aliyetenda dhambi? Yeye, ama baba yake, mama yake?"

53 Na Yesu akasema, "Katika kisa hiki, si hata mmoja wao; bali kwamba kazi za Mungu zifanywe, zijulikane."

54 Na kumbukeni, walisema ya kwamba baba na mama hawangeweza kusema. Wao walisema, "Wanajua huyu ni mwana wetu, bali hatujui jinsi alivyoponywa." Kwa sababu Wayahudi walikuwa wamesema ya kwamba mtu yeyote atakayemkiri Yeye kuwa ni Nabii, ya kwamba wangefukuzwa.

55 Lakini, unaona, kazi za Mungu zilikuwa ya kwamba mvulana huyu hakuwa wa kundi hilo. Naye alisema, "Sasa, ni ajabu kwangu ya kwamba hamjui Mtu huyu anatoka wapi, na hata hivyo alinifungua macho." Unaona? Sasa, angeweza kusema hilo. Unaona, hizo zilikuwa ni kazi za Mungu. Alikuwa ameponywa, na ni mzima, naye angeweza—angeweza kushuhudia kwa sababu hakuwa amefungwa kamba kutoka mahali popote. Alikuwa ndiye kazi hizo zilikuwa zimefanywa juu yake, na bila shaka alipata kuona ninii yake. . .kwa mara yake ya kwanza maishani mwake.

56 Sasa, Wayahudi waliungana pamoja dhidi ya Yesu na—na dhidi ya Umasihi Wake, na Ujumbe Wake wa Kimasihi. Tunaona jambo lile lile likitukia sasa, jambo lile lile tu. Ukomunisti unaungana kuliangamiza kanisa, na njia pekee ambayo. . .hiyo ni baada ya kanisa kujiunganisha pamoja pia, katika Baraza la Makanisa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, kuukana na kuuangamiza Ujumbe, Neno! Wamelikataa Neno, makanisa yamelikataa! Hawawezi kulikubali kwa sababu ni kinyume cha kanuni yao ya kimadhehebu; haidhuru ni Nguzo ngapi za Moto zingening'inia katika ninii yetu. . .miongoni mwa watu, ama ni watu wangapi wangeninii. . .ni mambo mangapi yangetabiriwa na yatukie, na ishara zote kuu ambazo Yeye aliahidi za siku ya mwisho; hawawezi kuamini.

57 Kwa hiyo, wanaungana pamoja sasa, na mchungaji wenu hapa na wengi wanaweza kuwaambia, wanaosoma, ya kwamba wao. . .wana mwenendo wa ekumeni wa u—u—ulimwengu. Na ninii. . .linaongozwa na mhudumu wa Kilutheri. Hilo, kama kukitokea maafa, yangetukia kwenye ujirani huu hapa; kama hatujaungana na mwenendo huo wa ekumeni, basi kanisa letu haliwezi tena kuwa kanisa, nao wanaweza kulitumia kama ghala. Ama kama mmoja wetu sisi ndugu angemwona mtu fulani akifa ama ameumia, na kujaribu kumhudumia baraka yoyote ya Kiroho, tungepigwa risasi kwa ajili ya jambo hilo; kweli kabisa. Tunaweza kupewa kifungo cha miaka kumi katika gereza la shirikisho kwa kuhudumia chochote, kwa kuwa sisi si wafuasi wa mwenendo huu wa ekumeni. Je! hamwoni ile alama ya mnyama? Unaona? Unaona?

58 Sasa, tunaona wakati huu wa kuungana ukija. Unaona? Sasa, angalia! Na halafu kanisa limejiunganisha lenyewe dhidi ya Ujumbe; na ndipo basi wakati linapofanya hivyo, mataifa yanaungana pamoja katika Ukomunisti yapate kuliangamiza kanisa tena; vile vile hasa lilivyofanya kwanza. Unaona? Inajirudia yenyewe moja kwa moja tena.

59 Ilibidi Israeli iukatae Ujumbe kwanza. Na hapo walipoukataa Ujumbe, basi jeshi, maisha ya kitaifa yenyewe yaliungana pamoja (ya mataifa mengine), wakaja wakaliangamiza kanisa. Na leo, wameukataa Ujumbe wa Bwana Yesu, nao wameukataa. Na sasa, wakati umewadia ambapo Ukomunisti unauunganisha ulimwengu pamoja dhidi ya kanisa. Unaona, haina budi kuwa hivyo. Sasa, ni vigumu kusema jambo hilo.

60 Ilikuwa ni vigumu kwa hao Wayahudi kuamini, walisema, "Sasa njoni, ndugu, tunaona ya kwamba—ya kwamba nanii wetu—Mungu wetu yuko pamoja nasi, na kwa hiyo tuta—tutaingia Hekaluni. Na sasa tutaomba, na tumwache baba mtakatifu *Nanii* na baba mtakatifu *Nanii*, aongoze katika maombi. Fungeni lango!" Ndipo Tito akawazingira, na kuwazingira pale kwa karibu mwaka mzima ama zaidi. Unaona, akashika zamu moja kwa moja, na kuwaua kabisa kwa njaa. Asingekuwako na hata mmoja wao angaliweza kutoka nje ya mji; nao wakafa, kufa kwa njaa. Na wakati alipoingia mle na kuzibomoa hizo kuta, damu ilifoka na kutiririka kama mito kule chini ambako alichinja kila kitu kilichokuwa mle ndani.

61 Sasa, Malaika wa Bwana alitabiri jambo hilo, huko nyuma katika Agano la Kale, na kusema kwamba hayo yangetukia. Na hao wahudumu waliokuwa makasisi, waliopaswa kujua hayo na kuwaambia watu hayo; badala yake, wakati Yesu aliposimama miongoni mwao, hata hawakumjua; na kujaribu kufanya na—na—namna fulani ya—ya vitimbi, "Tufanyie kitimbi, hebu tuone jinsi—jinsi kinavyofanywa! Tuonyeshe ishara." Unaona? Naye akasema, "Mimi. . ." Mbona, Yeye amefanya mambo mengi sana, na hata hivyo wasingeweza kuliona. Unaona? Na ndipo wakati walipomkataa kama nanii wao. . . Ujumbe wa siku hiyo, waliukataa Ujumbe wa siku hiyo.

62 Walishindwa kuona ishara ya siku hiyo. Na ishara ya u—unabii wa Biblia ilifanywa mbele zao, nao wakasema, "Hebu na tuingie sasa!" Hao walikuwa ni watu watakatifu. Walikuwa ni watu ambao usingeweza kuyaelekezea kidole maisha yao. Wasingeweza kuwa *hivyo*, na halafu—na halafu awe ku—ku—kuhani. Kuhani angaliuawa, angalipigwa mawe hata afe kwa jambo lolote dogo. Kwa hiyo ilibidi aishi maisha safi, matakatifu. Asingeliweza kulifanya, kwa kuwa alipigwa mawe kwa jambo lolote tu. Na sasa walikuwa ni watu mashuhuri, na watu watakatifu machoni pa watu, na hata hivyo waliingia na kusema, "Sasa, tutaninii. . . Tuna Mungu, Mungu ambaye amekuwa pamoja nasi katika nyakati zote. Tutaenda tuingie katika Hekalu Lake Takatifu." Hilo lilikuwa ni Hekalu Takatifu la Mungu! Lakini, unaona, Yeye alikuwa amekataliwa katika Hekalu Lake Takatifu. Unaona? "Tutaenda Nyumbani mwa Bwana. Sasa ninyi nyote Waebrania mnajua ya kwamba sisi ni jamii iliyochaguliwa, ndivyo tulivyo, hapa. Na Mungu ni Mungu

wetu; Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Yeye yuko pamoja nasi. Atatukomboa na hao Wafilisti wasiotahiriwa huko nje (tuseme), hao Warumi na Wayunani. Atatukomboa na hao. Haya twendeni Nyumbani mwa Bwana!"

63 Hilo linasikika zuri; lakini walikuwa wamefanya nini? Mwenye Kuijenga nyumba hiyo alikuwa mle ndani, katika namna ya seremala Mgalilaya mnyenyekevu, nao wakamkataa; wakati Mungu alikuwa amemthibitisha kwamba alikuwa ni Mjumbe Wake wa wakati huo, na tawi. Nao wakamkataa. Kwa hiyo kuomba kote, uaminifu wote, dhabihu zao zote hazikumaanisha kitu kwa Mungu. Walikuwa wamemkataa! Ndipo Mungu akaliacha jeshi hili kuu liungane na kuwaangamiza.

64 Nasi tunaona siku hizi, kama makanisa kupitia kwenye madhehebu na kadhalika, wakilikataa Neno la Mungu. Hawataki uwaambie kuhusu mambo haya, na sayansi inaweza kuyathibitisha kwa picha na chochote kile, na hata hivyo hawataki uhusiano wowote na Hilo. Kwa hiyo ukomunisti unajiandaa kuliangamiza, kama tu vile Tito alivyofanya, nayo Biblia ilisema wangeangamizwa. Kweli kabisa!

65 Sasa, unaona mahali tunapoishi? Wakati wa kuungana. Tunapoona mambo haya yakiungana, loo; mbona, tunashindwa kuona mambo hayo! Unaweza—unaweza kuangalia hapa katika Maandiko na kuona ambapo Yeye aliahidi hayo, yale atakayofanya. Sasa, tunaona jambo hilo likitimia. Tunaona kanisani lile aliloahidi kufanya; tunaliona likitimia. Tunaona mataifa yakiungana pamoja. Tunaona itikadi zikiungana pamoja. Tunaona makanisa yakiungana pamoja. Ni wakati wa kuungana. Ni majira ya kuungana. Hiyo ndiyo roho ya wakati huu, "Hatuna budi kuungana." Kila kitu unachozungumza habari zake hakina budi kuunganika; hata serikali haitakipokea.

66 Unajua, kama mwananchi . . . siwezi kama mwananchi, kama mwananchi wa Marekani, bali ni—ni . . . ungenipa hundi ya dola tano na nisingethubutu kuweka jina langu juu yake. Unaona? Unaona, nisingeweza kufanya hivyo. Unaona, ni wakati wa kuungana. Haina budi kupitia kwenye muungano wa namna fulani, na muungano huo ndio hasa unaoleta ile alama ya mnyama. Unaona? Ni wakati wa kuungana, na linaelekea moja kwa moja kutimiza jambo hilo. Unaweza kuliona kwa macho yako ya kawaida, ukiiangalia. Ni wakati wa kuungana, ambapo kila kitu kinaungana pamoja.

67 Myahudi—Wayahudi waliungana pamoja dhidi ya Yesu, kama nanii wao—kama Masihi wao. Kwa hiyo, tunaona ni jambo gani lililotukia. Tunaona jambo lile lile sasa, ukomunisti ukiungana kuliangamiza kanisa, baada ya kanisa kuungana katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni na kujaribu

kuuangamiza Ujumbe, Neno la Mungu. Walijaribu kuuondolea mbali. Jambo pekee wanaloweza kufanya ni kujiundia baraza fulani, kwa maana wametengana; kundi dogo hapa, Wamethodisti, na Wabaptisti, na Walutheri, na Wapresbiteri, kanisa la Kristo, na kadhalika namna hiyo. Hawawezi kufanya jambo lolote, kwa maana *hili* litapingana na h*ili*, *hili* litapingana na *lile* lingine, mafundisho yao ni tofauti sana kama mashariki ilivyo mbali na magharibi. Unaona, hawawezi kufanya jambo hilo. Lakini mara wakiungana pamoja, chini ya kiongozi mmoja mkubwa, wamefaulu. Wamefaulu basi.

68 Hapo ndipo Wakatoliki walipo katika umoja, Katoliki ya Kirumi, hakika wana umoja, wananinii . . . walio wengi sana ni Katoliki ya Kirumi; wa Kigiriki na Wakatoliki wengine si—si wengi kama Katoliki ya Kirumi. Sasa wanaungana pamoja, na hiyo ndiyo sababu wanasimama pamoja. Haidhuru ni jambo gani litakalotukia, huyo papa ndiye kichwa cha kila kitu. Unaona? Na haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, "Yeye hawezi kufanya makosa; yeye—yeye—yeye ni halifa wa Mungu, hivyo tu; ndiye wa pili kutoka kwa Mungu; ana mamlaka juu ya kuzimu, Mbingu, na toharani." Unaona? Kwa hiyo hakuna jambo linaloweza kufanywa katika jambo *hilo*; lolote asemalo, hilo ndilo halina budi kuwa.

69 Sasa, Waprotestanti wanajifanyia wenyewe kiongozi kama huyo, kabisa. Na si Biblia inasema kulikuwa na sanamu iliyofanyiwa mnyama? Sanamu ni nini? Ni kitu kinachofanana na huyo, kimetengenezwa kama yeye. Hiyo hapo, jambo lile lile. Ni kitu gani? Kwa kujiunganisha pamoja, na hii ndiyo roho ya wakati huu, ni *kuungana*.

70 Kuungana pamoja sasa, kujaribu kuuangamiza Ujumbe. Wanauangamiza namna gani? Wangewezaje kuliangamiza Neno la Mungu? Wanaweza kulitangua, lisiwe na nguvu, kwa kuchukua mapokeo kama walivyofanya huko nyuma, na kulitangua Neno la Mungu. Unaona, wanasema, "Aha, hilo . . . Kweli, kwa vyovyote vile, . . . " Unaona ambapo mwanamke huyu kafiri anayejaribu kuninii . . . yeye . . . ninasahau jina lake ni nani sasa; laiti ningaliweza kulitaja. Yeye . . . Ninajaribu kufikiria kuhusu wengi sana.

71 Ninawazia juu ya huyu Bibi Mataifa hivi majuzi; laiti tungalikuwa na mwingine kama huyo atakayeinuka. Yeye ndiye aliyeingia katika vilabu vya pombe na kurarua wiski, na kutupilia mbali vibao na kadhalika namna hiyo. Kwa nini mwanamke mwingine asiinuke leo namna hiyo, na kutoka nje hapa na kurarua baadhi ya picha hizi zilizo uchi za wanawake hawa wa jamii yake, na vitu kama hivyo? Hilo, hawana hao tena.

72 Sasa, lakini mwanamke huyu, kafiri, ambaye alisema ya kwamba—ya kwamba "Biblia inakiuka katiba, kuisoma katika shule za umma," na vitu kama hivyo.

73 Sasa wao pia je! umeona tena, wanajaribu kusema sasa, na wasomi mashuhuri wa Maandiko, walisema ya kwamba "mwingi wa unabii uliotolewa katika Biblia ulikuwa ni wa uongo kabisa, wala haukutimia." Nanyi mmesikia jambo hilo na kulisoma. Nao wanajaribu kusema kila kitu; unaona, wanajaribu kuangamiza ushawishi wa Neno hilo. Kama wanaweza tu kuliangamiza Hilo na kulibadilisha na kanuni fulani ya imani ama kitu fulani walicho nacho watu, ambacho kinaonekana kwa macho yao kuwa bora kuliko Neno, basi wanaliangamiza kwa ninii yao—mapokeo yao. Na hivyo ndivyo wanavyojaribu kuliangamiza Neno la Mungu, kwa siasa za kimadhehebu.

74 Sasa, kila kanisa lina siasa zake lenyewe. Kanisa la Kristo lina zake, kanisa la Kikristo lina zake, na Wabaptisti, na Wamethodisti, na Wapresbiteri; wote wana siasa zao mbalimbali. Sasa, wanaachilia hizo kwa sababu wametengana. Unaona, isingetendeka hapo nyuma, hawana budi kufanya hivyo sasa. Unaona, huu ndio wakati wa kuungana, na sasa wanayaweka yote pamoja na kuyaunganisha na waone watatokea na kitu gani. Jamani, ni kama kuoka mkate kutoka kwenye nyama ya farasi, na takataka kutoka kwenye kopo, na chochote walichokuwa nacho shirika; na kuvishindilia pamoja, na kutupa ndani viazi vichache vilivyooza na kadhalika pamoja, na kuona unaishia na kitu gani. Hakika sitaki chochote cha hayo. La, bwana! Hivyo ndivyo wanavyofanya. Unaona, wanawachukua watu wanaoamini ya kwamba Yesu alikuwa ni hadithi ya uongo, kanisa linaloamini ya kwamba Yesu alikuwa ni hadithi ya uongo; hao wengine, wengine wanaamini Yeye alikuwa ni Nabii.

75 Mmoja anasema, "Siku za miujiza zimekwisha."

76 Huyo mwingine alisema, "Huenda kukawa na kitu kama hicho."

77 Na yote haya pamoja; nayo Biblia ilisema, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?" Unaona? Sasa, hiyo ndiyo aina ya umoja walio nao. Na kumchukua baba mtakatifu fulani mkuu na kumweka juu yake, na hapo mna sanamu ya mnyama, jinsi hasa Biblia inavyosema. Sasa wana mhudumu Mlutheri, ndiye kiongozi wake. Vema, tunaona ni wakati wa kuungana. Jambo lile lile leo, Ukomunisti na wote wakiungana pamoja; ulimwenguni, na kanisani na kadhalika, wakiungana pamoja.

78 Angalia maumbile. Loo, jamani! Maumbile, kama utaliangalia tu maumbile, yanafanya jambo lile lile. Maumbile ni kalenda ya Mungu ya ishara. Hivi mlijua hilo? Yesu aliwaambia waangalie maumbile. Bahari itakuwa ikivuma, unaona, na kutakuwa na mambo mbalimbali, na matetemeko ya nchi mahali mahali, dhiki ya mataifa, ishara mbinguni, ishara duniani, kila mahali kutakuwako na ishara za nyakati hizi zijazo.

79 Angalia mawingu. Kabla mawingu hayajaweza kuleta mvua kubwa, mnajua jinsi inavyotendeka? Mawingu madogo kadhaa yanakusanyika, kufanya wingu moja kubwa. Vema, hili lina kusanyiko la pepo ndogondogo likilivumisha, hili lingine lina kusanyiko la pepo ndogondogo likilivumisha, na yote yanavuma pamoja, ndipo yana tufani. Unaona? Yanakusanyika kabla hayajaweza kupata dhoruba; hayana budi kuungana.

80 Angalia bata na bata bukini wakiungana pamoja kabla hawajaondoka nchini mwao. Unaona? Wanaungana pamoja. Unaweza kuwaona wakiruka kutoka kwenye kidimbwi hiki kwenda kwenye kidimbwi kile, kutoka hapa kwenda kule, wote wakikusanyika. Wanaungana, wakijiandaa kuruka. Unaona, ni ninii tu. . . hayo ni maumbile, na Mungu aliumba maumbile, na maumbile hutenda kazi kwa mpango wa Mungu. Ni sheria, sheria isiyoandikwa ya Mungu, kwamba maumbile hufanya kazi kulingana na amri Yake.

81 Ni kama tu, nilivyozungumza kwenye ibada ya mazishi, juu ya *utomvu* unaoingia kaburini, chini ya shina la mti, kukaa pale mpaka kwenye ufufuo katika msimu wa kuchipua. Ni sheria ya Mungu. Hakuna akili inayoweza kufanya utomvu huo kushuka kwenda kule chini; usingeweza kuutoa, usingeweza kuukamua. Hakuna njia ya kulifanya vizuri zaidi kuliko vile Mungu anavyofanya. Mungu ana njia kamilifu. Kwa hiyo wakati jani linapoanguka, ndipo Yeye hutuma utomvu chini ukaingia kaburini na kuuficha. Kama vile Ayubu alivyosema, "Nifiche kaburini mpaka ghadhabu Yako itakapopita." Unaona? Unashuka kwenda kule chini kwa sababu ni kanuni ya maumbile, kabla ya theluji nyembamba. Angalia majani sasa yakianza kuanguka. Kwa nini? Ni kanuni ya maumbile.

82 Mabata watakusanyika, kila mmoja wao, na kukusanyika chini ya kiongozi. Mle ndani watajua kwa namna fulani, sijui jinsi wanavyojua hilo, bali wanajua ya kwamba maskini huyo bata dume fulani ndiye kiongozi. Na maskini jamaa huyo, wote watakusanyika na kuungana moja kwa moja chini yake, na kupaa moja kwa moja hewani. Naye ataninii. . . kamwe hawajawahi kuondoka kwenye kidimbwi hicho sasa, lakini ataenda moja kwa moja mpaka Louisiana ama Texas awezavyo kwenda, kwenye shamba la mpunga. Unaona, kabla hawajaruka, kuacha makazi yao ambapo walizaliwa mwaka huo, wanaungana. Amina! Haya basi; wakiungana chini ya kiongozi wao.

83 Shida yake ni kwamba, kwa binadamu, yeye hamjui kiongozi wake. Naam, bwana. Watakusanyika chini ya dhehebu fulani, watakusanyika chini ya askofu ama mtu fulani, bali hawatakusanyika chini ya yule Kiongozi, Roho Mtakatifu katika Neno. Unaona? Wao wanasema, "Loo, vema, nahofu nitakuwa kidogo mshupavu wa dini; ninahofu nitaelekea kubaya." Loooo, haya basi! Vipi kama maskini huyo bata alisema, "Sipendi vile

anavyoweka manyoya yake. Siamini nitamfuata." Utaganda kwa baridi hata ufe. Utashikwa kule juu, kama hujiungi na—na safari hiyo ya hewani inapoondoka. Hujiunganisha pamoja, na maumbile hufanya hivyo.

84 Bata bukini huungana pamoja, wanakusanyika kumzunguka kiongozi wao; wanafanya jambo lile lile.

85 Je! ulipata kuona nyuki wakiparaga? Nyuki wataungana pamoja, kabla hawajaparaga, moja kwa moja wakimzunguka malkia wao. Hiyo ni kweli. Na mahali anapoenda, nao wanaenda pia. Naam! Wanafanya nini? Wanaungana kabla hawajaparaga. Kweli kabisa; kila maumbile!

86 Samaki huungana pamoja kabla ya mbio za majira ya kuchipua. Huko nje baharini, unaweza kuwapata; hao wakubwa . . . tunaowaita "vibiongo," salmoni. Wanapokuja kule juu, kabla ya hizo mbio kuanza, utawaona kwa makumi elfu, huko katika bahari hiyo, wakija wakizunguka-zunguka; maji ya chumvi, lakini kwa kweli wao ni samaki wa maji baridi. Na hawa hapa wanakuja moja kwa moja kwenye hayo maji baridi, wapande waende kwa ajili ya majira ya kutaga mayai kwa wingi. Wanapanda kwenda kule na kutaga, yapata kila baada ya miaka minne, kisha wanakufa mara tu wanapotaga mayai hayo. Nao wanajua wanaenda kule wapate kufa, wala usingeweza kuwazuia kwa chochote kile. Wataruka ngazi za samaki na chochote kile, wapande kule, wakijua wanaelekea kwenye kifo chao. Lakini kanuni ya maumbile inawafanya, wakijua wanapanda kwenda kule kutaga mayai shimoni, kisha wafe. Ndipo watoto wanatokea, na kitu fulani kinawaunganisha pamoja basi, na haoo wanaingia baharini. Ni kuungana! Ni kanuni. Huwezi kamwe kuishinda sheria ya Mungu.

87 Mataifa yana—yanavunjika, kwa ajili ya wakati sasa ambao tunaona ya kwamba—ya kwamba wanapaswa kufanya jambo hili. Tuko katika wakati wa vurugu za kitaifa. Tunaona mataifa yanavunja uhusiano. Mwaka baada ya mwaka, tunaona taifa *hili* likimezwa katika ukomunisti; *hili* likimezwa katika ukomunisti. Na papa hapa katika taifa letu wenyewe, limejaa ukomunisti, nao utaliteka! Unaona, utaliteka, hakuna njia ya kukomesha jambo hilo. Kwa nini? Sababu ile ile usingeweza kumkomesha Tito. Watu wamemkataa Mungu na Neno Lake. Naam, bwana, kwa hiyo wataliteka, na tunaliona moja kwa moja katika mchakato.

88 Mimi, kwa kawaida, mimi huchukua saa kadhaa; tayari nimechukua kama dakika thelathini, sasa hivi. Unaona? Lakini ili kuingiza haya yote ndani, ninasukuma tu. Yasomeni mtakapofika nyumbani.

89 Angalieni, sasa hivi wanaungana. Unasema, "Ndugu Branham, hiyo ni kweli?" Wanaelekea kwenye Vita vya Har-Magedoni; ndivyo hasa watakavyofanya. Unaona? Nao

wanaungana kwa ajili ya jambo hilo sasa hivi. Hiyo ndiyo sababu tuna U.M. na kila kitu tulicho nacho. Ulimwengu wa Magharibi unaungana dhidi ya ulimwengu wa Mashariki, ukomunisti na kadhalika, wote wanaungana pamoja. Makanisa yanaungana pamoja. Kila kitu kinaonekana kuungana. Kuungana, vikiungana vyenyewe kwa vyenyewe pamoja, tunaona jambo hilo.

90 Pia, wakati kuungana huku kote kwa taifa, ishara hizi, ishara za kitaifa, tunaona hapa nje ulimwenguni, matetemeko ya nchi mahali mahali, vitu mbalimbali vikiungana; vikiuleta ulimwengu pamoja, vikiwaleta watu pamoja, makanisa yote pamoja, mambo haya yote. Na wakati muungano huu wote ukiendelea, kuna muungano mwingine unaoendelea. Amina! Huo ndio ninaotaka kuwaonyesha sasa.

91 Mungu anamuunganisha Bibi-arusi Wake. Anakusanyika pamoja, kutoka Mashariki na Magharibi, na Kaskazini na Kusini. Kuna wakati wa kuungana, na huo unaendelea sasa hivi. Anaungana kwa sababu gani? Unyakuo. Amina! Mungu anamtayarisha. Naam bwana, kuungana! Anaungana na kitu gani? Na Neno! "Kwa maana mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Anajiunganisha Mwenyewe na BWANA ASEMA HIVI haidhuru madhehebu yoyote ama mtu yeyote mwingine anasema nini. Anajiunganisha Mwenyewe. Anajitayarisha. Kwa nini? Yeye ni Bibi-arusi. Hiyo ni kweli. Naye amejiunganisha pamoja na Bwana Arusi Wake, unaona, na Bwana Arusi ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

92 Nalo Kanisa na Bibi-arusi na Neno wanakuwa mmoja sana, mpaka Neno Lenyewe linatenda zile kazi za Bwana Arusi. Amina! Unaona jambo hilo? Kuungana! Sio tena, "Jiunge na kanisa"; sio tena *hili*, bali ni kukimbia kutoka kwenye kila kitu na kujifunganisha na Yesu Kristo. Unaona? Ni wakati wa kuungana. Mungu, akimuunganisha Bibi-arusi Wake pamoja, akimrudisha; kikamilifu kabisa. Akiunganisha Maneno ya ahadi Yake.

93 Wathesalonike wa Pili, mlango wa 2; inasema, mlango huu wa 5 unasema, "Watakatifu waliolala mauti katika mavumbi ya ardhi wataamka. Ndipo tutaungana nao (walio hai, pamoja na waliokuwa wamekufa), tutaungana kabla hata hatujafika Kule juu," maana Bibi-arusi atakuwa amekwisha kukamilika wakati atakapofika Kule. Wale walio hai, ambao wanajiunganisha na Neno, na wale waliolala tayari walifanya hivyo; na wote watakuja pamoja, wafanye muungano mmoja mkubwa wa kuungana kabla ya kupaa huko Juu. Amina!

94 Ukomunisti hauna budi kuinuka, mambo haya mengine hayana budi kuinuka, na kanisa halina budi kujiunganisha

lenyewe huko ng'ambo, wakati ninii. . .na mataifa huko nje kwa ajili ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni; na Bibi-arusi hana budi kujiunganisha Mwenyewe chini ya Neno la Mungu. Kusudi apate kufanya jambo hilo, Mungu ameshusha ishara ya Mbinguni na kadhalika, inayolithibitishia Kanisa, kama alivyolithibitishia taifa. Amina.

95 Mungu; wakati wa kuungana! Naam, bwana. Loo, jamani! Sasa, kumbukeni sasa, kuna kuungana kwa Neno (kuungana tena), kuirudisha "Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Kurudisha! Kwamba jambo hili lingalifanyika tu katika siku hii. Wakati tu lingaliweza kufanywa ni sasa hivi. Halijapata kushambuliwa mahali pengine popote; walienda kombo katika shamrashamra za kimadhehebu. Lakini sasa, si mali ya shamrashamra za kimadhehebu, kwa sababu ni wakati wa kuungana kwa wanaume na wanawake wa kila jamii, kila rangi, kila kanuni ya imani, kila kitu chini ya Kristo kwa Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kulirudia Neno.

96 Wakati wa kuungana kwa Kanisa! Loo, jamani! Kuunganisha kila Neno ambalo limetapanywa kila mahali na mashirika haya: tangu Nikea, Rumi, wakati walipoliundia kanisa la kwanza dhehebu, nao wakamuundia Luther dhehebu, wakamuundia Wesley dhehebu, wakaundia makanisa mengine yote madhehebu. Na kufanya hivyo, iliwabidi kuchukua kanuni ya imani, na halafu basi wakati Mungu alipotuma kitu kingine, wasingeweza kukipokea. Kwa hiyo, haikuwezekana mpaka wakati huu. Naye Mungu aliahidi, katika siku za mwisho, ya kwamba "Imani ya baba itarudishwa kwa Bibi-arusi tena," ya kwamba ingekuwa hivi, wala isingewezekana kuwa wakati mwingine wowote ila wakati huu. Angalia ni ishara ya jinsi gani kutoka Mbinguni, kama Nguzo ya Moto ikining'inia miongoni mwetu, na kukiweko na ishara na maajabu ya Bwana Yesu Kristo. Na wakati akizungumza na sisi, halishindwi kutimia kikamilifu kabisa juu ya alama. Amina! Ndipo tunaona mahali tunaposimama. Wakati wa kuungana!

97 Tunaona mataifa yakiungana, tunaona ulimwengu ukiungana, tunaona ukomunisti ukiungana, tunaona makanisa yakiungana; na tunamwona Mungu akijiunganisha Mwenyewe pamoja na Bibi-arusi Wake, mpaka Yeye na Kanisa ni kitu kimoja. Haleluya! Kama vile piramidi kule. Naam! Wakiungana pamoja; Mungu akiunganisha! Kwa nini? Mwali wa Moto, tangu wakati wa mwanzoni mwa kanisa, kamwe haujapata kuwa miongoni mwa watu. Tangu wakati wa mwanzoni mwa kanisa, hawajapata kuona mambo tunayoona leo. Na jambo hili liliwezekana tu wakati Mungu alipotuma ile Mihuri Saba na kutupa ishara kwa Hiyo, na akawatuma wale Malaika saba washuke chini kutoka Mbinguni; nao wakaja kurudisha Neno hilo lililotawanyika katika hayo madhehebu, na kulifunganisha

na Neno la Mungu tena, apate kumshusha Roho Wake Mtakatifu.

98 Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu likae ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Kumuunganisha tena Bibi-arusi kwenye Neno, ambalo ni Mungu. Kanisa na Neno, si Kanisa na kanuni ya imani, Kanisa na Neno; Bibi-arusi na Neno wakiunganishwa pamoja. Loo, jamani! Ni ninii. . .Kurudisha nini? Imani ya baba asili wa kipentekoste, unaona, iliyokuwa imetapanywa na kundi la Luther. Si Luther mwenyewe; si Luther, si Wesley, si wale waanzilishi mashuhuri. Lakini baada ya kuondoka kwao, kulikuwa na kanisa lililoibuka, nao. . .kile walichofanya na hilo basi, waliliundia dhehebu. Walikubali kanuni za imani na kadhalika, na haoo wakaenda. Na hebu waangalieni leo hii, sasa wameingia kwenye hilo Baraza la Makanisa Ulimwenguni.

99 Sasa, unaona, lakini katika siku za mwisho, unaona, tunaona mambo yakitukia sasa ambayo hayajapata kutukia hapo nyuma. Unaona, ni ishara ya Mungu, na kuungana huku kote ni ishara ya wakati. Sasa, tunataka kuangalia jambo hilo kwa makini na tuwe na hakika kabisa ya kwamba tunalipata. Wakiacha. . . wanaliacha Neno la kweli kuyaendea madhehebu; kukubali kanuni ya imani na maoni ya watu mbalimbali badala ya kulichukua Neno.

100 Ufunuo 10 ilisema, "Ujumbe wa malaika wa Saba." Sasa kumbukeni, hiyo ni moja kwa moja kwenye zile Baragumu Saba, na kuna malaika Saba wanaopiga zile Baragumu Saba. Hilo ndilo tunaloliendea baadaye. Lakini kumbukeni pale, kwa udhahiri sana Lilisema, "Ninii ya malaika. . .," si Baragumu ya malaika wa saba, bali "Ujumbe wa malaika wa saba." Unaona, si yule malaika wa Baragumu, yule malaika wa Ujumbe! Mnaona, malaika alipiga tu Baragumu, huyo malaika wa saba, malaika wa Baragumu. Lakini hili linasema, "Katika siku za Ujumbe wa malaika wa saba," unaona, wakati Ujumbe wake utakapomalizika. Unaona, huo ni Ujumbe wa wakati wa kanisa. Kwenye wakati huu, ndipo yeye angeninii. . .Ujumbe, si Baragumu, na "siri ya Mungu (ambayo imeandikwa katika Neno) itatimizwa."

101 Sasa angalia ni siku ya jinsi gani tunayoishi! Iangalie hiyo Mihuri, jinsi hiyo ilivyolivuta hilo Neno la Mungu lililotawanyika, lile Luther na hao wengine wote, ambalo hao watengenezaji mashuhuri waliotoka wakaenda; ikarudi moja kwa moja na kuonyesha jambo hilo katika Biblia, mahali watakapokuwa; kila mtu moja kwa moja katika mahali pake, jinsi ambavyo angefanya na kile kingelitukia kwa kanisa; kile ambacho yeye angefanya, na kile ambacho kingelipata kanisa; mambo haya yote aliyoyaacha. Halafu basi, katika siku ya mwisho, ambapo hatukujua kitu juu ya jambo hilo, ikatutabiria juu ya jambo fulani kutukia; na hata magazeti na kadhalika

yakachukua jambo hilo, kisha akashuka moja kwa moja na kulifunua na kuzifunganisha zile siri pamoja. Amina! Ndugu, hilo ni adhimu kwangu! Hilo, kwangu mimi, linaambatana na Neno. Sijali ni nini—nini . . . ama ninajali vile watu walivyosema, wanavyofikiri, hiyo ni kweli, bali kwangu mimi ni Kweli, ninaamini hilo.

102 Kama vile wale mamajusi, wakishuka kuja kutoka Babeli, walipiga makelele, "Yuko wapi Yeye; aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Yeye yuko duniani, sasa hivi. Hatuna budi kumpata." Hiyo ni kweli. Nami ninaamini Yeye yuko karibu sana na kuja hata ninaweza kusema, "Tazama, Bwana Arusi yuaja! Ninasikia kile kilio cha usiku wa manane!" Amina! Tuko kabisa kwenye wakati wa mwisho. Loo, jamani, saa tunayoishi. Angalia. Unaona?

103 Ni siku ya jinsi gani! Ni wakati wa jinsi gani tunaoishi, siri hii kuu ya Mungu ikitimizwa; ikileta Uungu, ikionyesha kwamba ni Nini; jinsi ambavyo itikadi hizi ndogondogo, na wakaenda kombo na kumfanya Yeye *hiki*, na mtu fulani akamfanya *hiki*, na mtu fulani akamfanya *kile*. Lakini Malaika wa Bwana alishuka na kuweka wazi itikadi zao zote, na akavuta akatoa ule Ukweli wa jambo hilo, na kuuweka wazi. Na huo hapo, kikamilifu tu uwezavyo kuwa, hakuna njia nyingine ungaliweza kupitia. Huo hapo, hivyo ndivyo Yeye alivyo. Unaona, uzao wa nyoka, mambo haya yo—yote mbalimbali ambayo yamekuwa ni siri sana miongoni mwa watu. Unaona? Ni kitu gani? Alikuwa . . . Hii ni ishara ya kufanya nini? Kuungana!

104 Alisema nini katika Malaki 4? Angerudisha! Kurudisha Imani ya mwanzoni ya kipentekoste, awarudishie watu ikiwa na Ujumbe ule ule wa kipentekoste, ishara ile ile ya kipentekoste, ushahidi ule ule wa kipentekoste, Mungu yeye yule, Nguvu zile zile, fundisho lile lile, kila kitu vile vile hasa, pamoja na thibitisho la Nguzo ile ile ya Moto iliyomwangusha Paulo chini barabarani, akishuka kwenda Dameski; miongoni mwetu leo, ikifanya mambo yale yale Yeye aliyofanya katika siku ile. Kuungana!

105 Tunaona mataifa yakiungana, tunaona ulimwengu ukiungana, tunaona makanisa yakiungana. Tunaona Bibi-arusi akiungana, akiungana na Neno. Kwa nini? Neno ni Mungu. Na kama Neno . . . Kama vile Bwana Arusi (akiwa ni Neno), na Bibi-arusi (akiwa ni msikiaji wa Neno), wanakuja pamoja katika Muungano. Wanaungana kama vile arusi. Unaona, wanajiandaa kufanya arusi, nao—nao wanakuwa mmoja. Neno linakuwa wewe, wewe unakuwa Neno. Yesu alisema, "Katika siku hiyo mtaijua. Yote aliyo Baba, ndivyo nilivyo Mimi; na yote niliyo Mimi, ndivyo mlivyo ninyi; na yote mliyo ninyi, ndivyo nilivyo Mimi. Katika siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba Yangu, Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Unaona? Katika "siku hiyo." Siku gani? Leo hii!

Tunaona zile siri kuu zilizofichwa za Mungu zikifunuliwa. Loo, jinsi ninavyopenda jambo hilo!

106 Loo, angalia jinsi ambavyo sayansi na Neno visingeweza kulinganishwa, kama wanavyofanya leo. Wasingeweza kufanya hivyo hapo kabla. Ni sasa hivi tu ambapo wangeweza kufanya hivyo.

107 Angalia, Yeye alisema, "ishara za mbinguni, ishara za mbinguni." Sayansi, na ishara za kitaifa; sasa wana ishara kuu mbinguni siku hizi, wana wanaanga na kila kitu. Lakini wanaanga hawa wanaufanyia nini ulimwengu wa sayansi? Inawaletea hofu. Hawajui ni wakati gani wangetuma kitu huko juu namna hiyo na kuangusha tu hizi bomu, nasi hatungekuwako tena. Unaona? Sasa hizo ndizo ishara walizo nazo, mambo ya kutisha mbinguni. Unaona? Wanazo, makombora ya atomiki na kila kitu, kila namna ya ishara.

108 Unaona ambapo walitia sahihi huu—huu mkataba, hivi majuzi, ya kwamba hawatalipua mabomu mengine juu ya nchi, bali sasa wanaingia chini ya maji na chini ya ardhi, wakiyajaribia vivyo hivyo. Unaona? Wanatia sahihi mkataba, "Hatutafanya hivi, kama ninyi mkisema hamtalifanya (bali tutarudi nyumbani na kulifanya hivi; wakati tunajua ninyi mnafanya vivyo hivyo huko kwenu)." Unaona? Hakuna chochote kabisa, ni ninii tu. . .hakuna kuaminiana kati yao, hakuna—hakuna chochote. Unaweza. . .Unaona? Na kila mtu anamwogopa mwingine. Hiyo ni ishara ya kutisha.

109 Sayansi na mwanadamu na mataifa wametengeneza ishara ya kutisha mbinguni. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, kuogopana mmoja na mwingine. Na kumekuwa na ishara ya mbinguni iliyotolewa kwa. . .Unaona sasa, wana ishara mbinguni pia, ishara ya kutisha, mwanadamu katika mwanaanga; huenda akawa na kombora la atomiki, na angeweza kuliangusha na kuliangamiza taifa zima. Apande juu katika mwanaanga, na kusimama huko nje. Hakuna kitu kinachowazuia wasifanye jambo hilo. Hakika wanaweza kulifanya, wao. . .wakati wowote wanaotaka. Wanaweza kuifanya mavumbi kama wangalitaka kufanya hivyo, lakini. . .katika dakika kumi na tano tangu sasa. Na kile mmoja anachoweza kufanya, huyo mwingine ni vivyo hivyo, pia. Kwa hiyo, unaona ya kwamba wana ishara, bali ishara ya namna hiyo inawafanya kuogopa.

110 Wanaungana pamoja, wakiweka nguvu zao pamoja. Ulimwengu huru, wanaweka nguvu zake pamoja. Ukomunisti unaweka nguvu zao pamoja na Urusi. Kila mtu; lakini kila mmoja anamwogopa mwenziwe. Unaona, ni ishara ya kutisha. Hiyo ni kweli. Hizo ni ishara za kitaifa, na kadhalika.

111 Bali Kanisa limepokea Ishara ya Mbinguni: Mwanaanga! Amina! Yesu Kristo, katika umbo la Nguzo ya Moto; aliyokuwa katika Agano la Kale, aliyokuwa wakati alipokutana na

Sauli akienda zake huko Dameski, Yesu yeye yule hapa leo! Na hiyo inafanya nini? Je! inaleta hofu? Inaleta upendo, unamuunganisha mtu mmoja kwa mwingine. Amina! Kujaliana. Inaleta Upendo wa Mungu, loo, ukituunganisha na kutuleta, Mwili wa Kristo, kuwa katika umoja kama Bibi-arusi. Hivyo ndivyo unavyofanya sasa, muungano huu mkubwa ambao Mungu . . .

112 Wanaungana pamoja, kundi moja *hapa* kupiga vita lingine, kundi moja *huku* kupiga vita hilo lingine. Hili hapa kanisa limesimama kati yao; hebu angalia linalotukia, litaungana nao. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini, sasa, tunaona ya kwamba hilo linasababisha hofu na mahangaiko.

113 Lakini Kanisa, Bibi-arusi, ameunganishwa na Mungu mmoja, chini ya Roho mmoja, Roho wa Mungu, katika Muungano mmoja Mtakatifu wa Mungu, lipate kuwa Bibi-arusi mmoja mtakatifu kwa Mungu. Hiyo ni kweli, kwa jumla; umoja wa ule Mwili. Ule Mwili ukingojea kama Bibi-arusi; kwa—kwa kuwa ni Bibi-arusi, kama tunavyojiita wenyewe Bibi-arusi. Kwa ajili ya wakati wa kuungana kwa Bibi-arusi, Kanisa linaungana. Inapaswa kuumba upendo tu miongoni mwetu, hata ingekuwa ni vigumu kuachana. Hiyo ni kweli. Tunaninii tu . . . haikubidi kuwasihi watu waombe, haikubidi kuwasihi wamwabudu Mungu, haikubidi kuwasihi kufanya yanayofaa. Wao wanampenda sana, hata hakuna jambo lingine.

114 Unawazaje juu ya msichana mdogo, maskini mwanamwali mdogo mrembo kweli, ambaye anataka kuolewa na kijana mwanamume mwenye sura nzuri ambaye anampenda kupindukia, inamaanisha ya zaidi kwake kuliko uhai wake mwenyewe, naye anajua pasipo kuchelewa ya kwamba watafunga ndoa. Wakati siku hiyo ya arusi inapokaribia, maskini jamaa huyo, nawaambieni, yote anayofanya ni "kuzunguka-zunguka." Unaona? Yeye anaandaa kila kitu; anajisalimisha kabisa kwake. Hiyo ni kweli. Kila kitu kinachomfurahisha, hicho ndicho tu anachotaka kufanya. Vema, hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa leo hii, kwamba maisha yetu yanapaswa kufichwa sana katika Mungu kwa njia ya Kristo, kutiwa muhuri mle ndani kwa Roho Mtakatifu.

115 Jambo ambalo nimekuwa nikiwafundisha hapa, ni kuwaambia ishara hizi na mambo mbalimbali yanayotukia, sina wakati wa kufanya hivyo sasa; nitafanya hivyo katika ujumbe mwingine, Bwana akipenda. Lakini kuna kitu kimoja kidogo kinachokosekana Kanisani bado. Nasi tunakitaka hicho, kukifikia hicho, nami niko kabisa ukingoni mwake sasa. Unaona? Tunataka kukifikia hicho, kama . . . huna budi kukifikia. Usipokifikia, ni hayo tu, huna budi kukifikia. Kwa maana angalieni, wakati wa kuungana umewadia, kwa kuwa Mungu analiunganisha Kanisa pamoja lipate Ku—Kunyakuliwa liende kwenye arusi kwa ajili ya ule Muungano Mkuu: wakati

Mungu na mwanadamu wataungana katika Umilele, wakati viumbe vya wakati vitakapoungana na aliye wa Milele.

116 Ilifanywa wakati mmoja katika umbo la Mwana wa Adamu hapa duniani. Naye ilimbidi kuyatoa Maisha Yake apate kuleta nguvu fulani, kuwaunganisha watu wengine na Nguvu ii hii, kwa ajili ya Bibi-arusi wa Yesu Kristo. Na sasa Kanisa linajiunganisha kwenye Mwili wa Kristo. Limejiweka huru, likajikatilia mbali na kila pingu ndogondogo, likijiandaa; likikusanyika pamoja, muungano miongoni mwao; loo, upendo na furaha, na Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwao. Loo, jamani, ni wakati wa jinsi gani!

117 Tunapoona mabata wakijitayarisha, tunawaona bata bukini wakijiandaa, tunawaona wanyama. . .nyuki wakijiandaa, tunaona mawingu yakijiandaa kwa ajili ya mvua, tunaona kila kitu; jinsi kinavyojiunganisha pamoja, kwa ajili ya msukumo wake mkuu. Tunaona Shirikisho la Mataifa, la mataifa pamoja, yakijiunganisha katika ukomunisti. Tunawaona wakiungana hapa katika Ulimwengu wa Magharibi. Tunaona kanisa likijiunganisha pamoja, hawa wengine wote. Kwa hiyo haiwezekani kabisa, hakuna wakati mwingine ambapo lingeweza kuwa hivi; isingeweza kuwa hivi miaka ishirini iliyopita, isingalikuwa hivi. Isingalikuwa hivi miaka kumi iliyopita, haina budi kuwa ni sasa hivi. Unaona, kwa sababu itikadi hizi na kadhalika hazikuwa zimefika mahali hapa.

118 Sasa amkeni! Jitikiseni, upesi sana, na mwangalie hapa mahali tulipo! Tuko wapi? Kama wale mamajusi, tuko moja kwa moja tumejipanga na Neno Lake, na Nuru ya Bwana inaimulika njia yetu. Utukufu kwa Mungu Aliye Juu Sana. Na Utukufu kwa Mungu aliyetupa Yesu Kristo, ambaye tunampenda, na ametuleta mahali hapa. Na tunaponinii. . .Sisi ni watu Wake, tulionunuliwa kwa gharama ya Damu Yake.

119 Loo, jamani! Hapo wakati wa kuungana utakapokuja, tunatazamia, kama tulivyoungana sisi kwa sisi katika vifungo vya Roho Wake, sisi. . .Je! inaweza kuwa ni Roho Wake? Hakika, ni Roho Wake. Kwa nini iwe Ndiye? Ni Neno Lake, na Yeye ni. . .huyo ni Roho wa Neno. Na wakati Roho huyo wa Ahadi anapokuja juu yako na kujithibitisha na kujionyesha Mwenyewe papa hapa, je! Yeye ni Roho yeye yule? Ndiye aliyekuwa pamoja na Musa huko nyikani! Ndiye aliyekuwa kwa Yesu Kristo! Ndiye aliyekutana na Sauli akienda zake Dameski! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Naye anafanya jambo lile lile!

120 Nasi tunaona mataifa pamoja, tunaona makanisa yakielekea upande mmoja pamoja, tunaona ukomunisti pamoja, tunaona itikadi zikiungana, tunaona mambo haya yote; na sasa tunaona Bibi-arusi akiungana na Neno. Loo, jamani! Wakati umewadia ambapo watakatifu watafufuka na kuungana na wale walio hai, wapate kwenda wakaungane na Yesu Kristo Milele.

121 Mungu na atusaidie, kila mmoja, kuungana na Kristo usiku wa leo, wakati tutasalimisha vitu vyetu vyote tulivyo, kila kitu tulicho nacho, nafsi yetu yote, mwili, na nia zetu kwa Yesu Kristo, na tuutazamie wakati huo wa kuungana huko.

> Parapanda ya Mungu itakapolia, na hapatakuwako na wakati tena,
> Na asubuhi ipambazuke ya Milele, yenye kung'aa na nzuri;
> Wakati waliokufa katika Kristo watakapofufuka na kukusanyika kwenye pwani ya pili huko ng'ambo (pamoja na Bibi-arusi aliye hai), wakanyakuliwe pamoja.

122 Angalia huko kuungana! Mungu analiunganisha Kanisa na Neno Lake, Neno na Kanisa, kusudi wote wawili wawe ni mmoja, "Sema *hili*, na litatukia. Fanya *hivi*, na litatendeka. Jambo ndilo hili; huyu ni Mimi mbele yenu, huyu ni Mimi nikilithibitisha; huyu ni Mimi pamoja nanyi." Vema.

123 Tunaona ya kwamba sasa wakati unawadia ambapo Parapanda italia, na wale watakatifu waliolala huko nyuma, ambao wasingekamilishwa bila ya sisi; wanatutegemea sisi (Waebrania 11); na wakati watakapokusanyika, wataungana na walio hai. Kanisa likiungana na Neno, ndipo Kanisa na Neno pamoja vinaungana, vikifanyika mmoja. Watakatifu waliokufa na watakatifu walio hai wakiungana pamoja kuwa mmoja; na wote wakienda pamoja kuungana na Kristo huko ng'ambo, kwa ajili ya Karamu ya Arusi ya Mwana-Kondoo.

124 Ni wakati wa kuungana, na ishara zinapepea kila mahali. Ishara ziko katika mataifa, ishara ziko katika ukomunisti, ishara katika Ulimwengu wa Magharibi, ishara katika Baraza la Makanisa. Na Ishara iko hapa usiku wa leo chini ya himaya ya Roho Mtakatifu, na Neno la Mungu linaithibitisha na kuifanya Kweli. Amina! Wakati wa Kuungana! Ishara ya Wakati wa Kuungana!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

125 Bwana Yesu, wakati maskini moyo wangu ukiruka kwa furaha, ninapoona uwezekano, (wa mimi mtu wa makamu), bali hata hivyo uwezekano wa mimi kukuona ukija katika kizazi hiki; kuwa hai na kusimama hapa, na kuona wakati ile Parapanda ikilia, "Aliye mchafu, angali ni mchafu. Aliye mwenye haki, angali anatakaswa. Aliye mtakatifu, angali ni mtakatifu." Ee Bwana Mungu!

126 Na kuwazia juu yetu tukisimama, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, wakati ulimwengu hautajua kile kinachoendelea, bali kwa ghafla, utawaona wapendwa wako waliokuacha, wakitokea mbele yako, wamekuja kuungana nawe tena. Nasi tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho; na kutwaliwa juu, pamoja, kumlaki Bwana

wetu hewani. Halafu tuungane Naye, tupate kuwa huko milele, wala tusilazimike kuondoka Mbele Zake tena.

127 Ni jambo kubwa lililoje leo, Bwana, kujua ya kwamba sasa tumeungana kama Roho mmoja. Roho mmoja, Roho Mtakatifu, amelishika Neno mkononi Mwake, akija ndani yetu. Na ni jambo kubwa jinsi gani, ni baraka jinsi gani kujitenga na ulimwengu wote, kujiunga pamoja na Yesu Kristo. Na kuwazia ya kwamba siku moja, katika mwili wa nyama, tukiwa na mwili kama mwili Wake wa utukufu, tutaketi mezani kwenye Karamu ya Arusi na hapo tuungane na kufunga ndoa pamoja Naye; tupate kuishi kama Bibi-arusi na Bwana Arusi katika nyakati zote zijazo, katika Umilele usio na mwisho.

128 Bwana Mungu, jalia hili lisiwe ni wazo tu la uongo kwa watu, bali jalia liwe halisi sana hata njaa na kiu zitawashika watu mpaka wataninii. . . wakisoma magazeti yao, wakiangalia. . . wakisikiliza redio na taarifa za habari, na kuona ni wakati wa kuungana. Ishara zinamulika.

129 Bwana Mungu, kama tulivyozungumza juu ya wanawake, yale wangefanya katika siku za mwisho; vile kanisa lingefanya katika siku za mwisho; na vile Nyakati za Kanisa zingekuwa, na vile Mihuri ingekuwa, mambo haya mengine yote. Na tunaona kama ilivyokuwa, katika siku za Nuhu. Tunaona kama ilivyokuwa, katika siku za Sodoma na Lutu, wakati Malaika wa Mungu alipojitambulisha katika mwili wa kibinadamu, aliyekula nyama ya ng'ombe na kunywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na kula mkate; na kusimama pale na angeweza kujua kile kilichokuwa kikitendeka nyuma Yake. Naye Yesu alisema jambo lilo hilo litatukia wakati wa kuja kwa Mwana wa Adamu.

130 Bwana Mungu, tumeona piramidi, jinsi tulivyoijenga kule, na tumeona jinsi tulivyoongeza vitu hivi kwake; na kuona kwamba tuko katika wakati wa mwisho, tukingojea Jiwe Kuu la Pembeni. Utukufu kwa Mungu! Tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawaamsha watu, upesi sasa, na kutukusanya pamoja, kwa upendo wa kiungu na heshima kwa Yesu Kristo na mmoja kwa mwingine.

131 Kama kukiweko na wengine hapa usiku wa leo wasio na hilo tumaini lililowekwa ndani yako, waweza kumwinulia Mungu mkono wako na kusema, "Bwana Mungu, niunganishe na Wewe, niunganishe na Wewe"? Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki, na wewe, wewe; naam. "Niunganishe na Wewe, Bwana." Naam! Loo, jamani!

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,

132 Waangalie Israeli kule, wameungana pamoja. Israeli, kutoka kote ulimwenguni, wamekuja kuungana; kuungana na sasa wao ni taifa. Wao ni taifa lililoungana: wakiwa na bendera yao wenyewe, fedha zao, jeshi lao, kila kitu; kama walipata kuwa, ndivyo walivyo sasa. Israeli imeungana, Roma imeungana,

kanisa limeungana. Na Bibi-arusi anaungana, amina; na kule kuja kwa ule Muungano Mkuu. Ni kitu gani? Yote inaelekea kwenye ile Ishara, ile Ishara muhimu sana, Yesu na Bibi-arusi Wake wakiungana kama mmoja.

133 Baba, Mungu, tujalie baraka hizi ninazowaombea watu hawa, na jalia tuungane na Wewe moyoni na katika roho, wanapoinua mikono yao, wakitamani jambo hilo. Bwana Mungu, tusafishe na utufanye kuwa Wako; tujalie hayo, Bwana. Hivyo tu ndivyo tujuavyo na tuwezavyo kufanya, ni kuomba. Halafu ulisema kama tuliomba jambo na kuamini, yatupasa kulipokea; ninalitazamia, Bwana. Ninakushukuru katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari. (Amina. Loo, jamani!)

Tazama, Bwana Arusi yuaja!
Ninasikia makelele ya usiku wa manane!
Tutapanda juu kwa sauti kuu, kama sote tukishikilia,
Na kumlaki Yeye hewani.

Kesha ukiomba, ndugu yangu,
Mtu asije akachukua taji lako,
Kwa maana mwenye uvuguvugu na aliyerudi nyuma
Hawatavaa joho la arusi.

134 Hiyo ni kweli. Na tuwe tayari kwa ajili ya makelele haya ya usiku wa manane. Yanakuja katika saa usiyowazia. Kutakuwa na makelele, si miongoni mwa ulimwengu usioamini; itakuwa ni siri. Lakini waaminio, wanaotazamia jambo hili, je! mnaona nyota zikipanga mstari? Unaona? Ilisababisha kitu gani? Kama tu ilivyofanya mara ya kwanza. Unaona, sisi hapa, ishara zinakuja.

Tunaona ishara zikitokea za Kuja Kwake kwenye baraka,
Tazama, majani ya mitini yakiwa kijani;
Injili ya Ufalme imeingia katika kila taifa;
Nasi tuko karibu, mwisho unaweza kuonekana.

Ndipo kwa furaha, mbali, tutautangaza Ujumbe wa kutokea Kwake kwenye baraka,

135 Hiyo ni kweli? Loo, na tupige mbiu za Ujumbe wa kutokea Kwake kwenye baraka! Hivyo ndivyo itupasavyo kufanya. Kumwambia kila mtu, “Jiweke tayari, iweni tayari kumlaki Mungu.” Amina! Ninampenda. Loo, jinsi ninavyompenda. Sasa, hebu tusimame kwa miguu yetu sasa. Tunapoagana sisi kwa sisi, nyosha mkono ukampe mkono mtu fulani, na kusema:

Hata twonane! (peaneni mikono, sasa) . . . hata twonane!
Hata twonane miguuni pa Yesu;
Hata twonane! . . .

Kumbuka, huenda ukapata wito. Huenda ikawa tutakapokutana tena itakuwa ni miguuni Pake.

Ee Mungu awe nanyi hata twonane tena!

136 Sasa, wazia tu, kabla hatujakutana tena; kabla hatujakutana Jumapili asubuhi, ama Jumatano usiku, huenda ikawa kwamba . . . muda si muda wajua, mtu fulani hayuko. Huyu hayuko, nao wametuacha. Loo, kuwazia juu ya mume wako kukuacha, ama mke wako kukuacha, na—na mke wa Yohana kukosekana, na—na—na huku watoto hawako. Yote yalitukia (ni jambo gani lililotukia?), ndipo umeachwa nyuma!

Loo, ni kilio na maombolezo ya jinsi gani wakati waliopotea watakapoambiwa mwisho wao,
Waliililia miamba na milima, (kama vile Israeli, wakirudi mjini, wakaingia Hekaluni.)
Waliomba lakini maombi yao yalikuwa yamechelewa mno. (Waliukataa Ujumbe.)

137 Loo, ndugu, kamwe usifanye hivyo. Lolote ufanyalo, simama kishujaa kwenye huduma! Naam, bwana!

138 Sasa, hata twonane, tutafanya hivi:

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila tatizo;
Majaribio yakikuzingira, (Unafanya nini?)
Litamke jina hilo takatifu maombini.

Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

139 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapouvumisha.

Tunasujudu kwa Jina la Yesu,
Tutasujudia miguuni Mwake;
Mfalme wa wafalme Mbinguni . . . tutamvika taji,
Safari yetu itakapokamilika. (Itakuwa hivyo, siku moja.)

Jina la thamani, Jina la thamani, ni tamu jinsi gani!

Hata twonane tena, Mungu awe nanyi.

Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, ni tamu jinsi gani! Tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

*Wakati Wa Kuungana Na Ishara Yake* SWA63-0818
(The Uniting Time And Sign)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 18 Agosti, 1963, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org